# Kamati: Kiwanda cha ngozi Kilimanjaro kuongeza ajira

**Na Mwandishi Wetu,**
MOSHI

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, imeridhishwa na maendeleo ya mradi wa kiwanda cha bidhaa za ngozi cha Kilimanjaro, ikieleza kukamilika kwake kutachochea upatikanaji wa ajira na kuondokana na uagizaji wa viatu visivyo na ubora nje ya nchi.

Kiwanda hicho kinamilikiwa kwa asilimia 86 na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), na Jeshi la Magereza linamiliki asilimia 14.

Akizungumza jana, baada ya kukagua kiwanda hicho katika Manispaa ya Moshi, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Fatuma Toufiq, amempongeza Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kusimamia kwa dhati dhana ya uchumi wa viwanda.

Alisema kuwa soko la ndani la viatu kama litakuwa kubwa, uagizaji kutoka nje ya nchi wa viatu vyenye ubora wa chini nao utapungua.

"Tutaishauri serikali kuendelea kuweka fedha za kutosha kuhakikisha uzalishaji unakuwa endelevu. Tunaposema tunaelekea uchumi wa viwanda miongoni mwa viwanda vitakavyokuwa bora Afrika kiwe ni kiwanda hiki nchi za SADC (Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika), Jumuiya ya Afrika Mashariki ziagize kutoka hapa kuongeza upatikanaji wa ajira," alisema.

Mjumbe wa kamati hiyo, Almasi Maige na Neema Lugangira, kwa nyakati tofauti, wameipongeza serikali kwa uwekezaji huo na kushauri kujitangaza na kupanua wigo wa upatikanaji wa wateja wa makundi mbalimbali kutokana na ubora wa viatu hivyo.

Baada ya ukaguzi huo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, aliahidi serikali itaendelea kufanyia kazi ushauri wa kamati kwa kuwa kipaumbele kikubwa cha Rais Samia ni kuleta ustawi wa Watanzania.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Ofisi hiyo, Patrobas Katambi alisema soko la viatu limeendelea kuimarika na kwa sasa kuna taasisi nyingi za serikali zinachukua huku mikakati ikiendelea kuhamasisha taasisi zingine kuchangamkia viatu hivyo ambavyo vina ubora unaotakiwa.


Awali, Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Hosea Kashimba, aliieleza kamati hiyo kuwa gharama ya uwekezaji wa mradi huo hadi utakapokamilika inakadiriwa kufikia Sh.bilioni 152.96.

Kwa mujibu wa Kashimba, mradi huo unatarajiwa kurudisha gharama zake ndani ya miaka 10, kuanzia pale mradi utakapokamilika.

CamScanner

KAMPENI

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Mkaranga, akiwa katika ziara ya kukagua miradi ya maendeleo, wilayani Ruangwa, mkoani Lindi, jana. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu).



# Majaliwa awageukia wafugaji

Na MWANDISHI MAALUMU, *LINDI*

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema kitendo cha wafugaji kuingiza mifugo katika mashamba ya wakulima ni uvunjaji wa sheria.

Amesema serikali haitovumilia vitendo hivyo huku amewataka wafugaji wafuge mifugo yao, kulingana na ukubwa wa maeneo yao ya malisho.

Majaliwa alisema hayo wilayani Ruangwa mkoani Lindi jana, alipozungumza na wananchi katika Vijiji vya Nanjaru na Mkaranga vya Kata ya Nambilanje na Nankonjera kilichopo Kata ya Namichiga akiwa katika ziara ya kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa wilayani humo.

"Kilimo ni maisha, kilimo ni biashara, kilimo ni fedha, vivyo hivyo ufugaji ni maisha, ufugaji ni biashara na ufugaji ni fedha hivyo kila mkulima alime kulingana na ukubwa wa eneo lake na mfugaji afuge mifugo kilingana na ukubwa wa eneo lake na malisho. Sisi sote ni Watanzania na tunataka utajiri. Wakulima na wafugaji waheshimiane kwani wote ni Watanzania,"alisema.

Alisema migogoro baina ya wakulima na wafugaji, haina tija na serikali haitaki kuiona ikiendelea na kwamba, kati yao, hakuna mwenye haki zaidi ya mwingine, hivyo kila mmoja aweke mpango kazi ambao hautaathiri upande wowote.

Waziri Mkuu, aliwataka watendaji wa vijiji kabla hawajagawa maeneo kwa wafugaji, wahakikishe idadi ya mifugo waliyonayo na washirikishe Serikali ya Kijiji na wananchi.

"Wafugaji badilikeni, fugeni kisasa, msione fahari kuwa na idadi kubwa ya mifugo ambayo mnashindwa kuihudumia. Fugeni mifugo michache ambayo mtaihudumia vizuri na kuiuza kwa gharama kubwa,"alisema.

Katika hatua nyingine, Majaliwa alitoa wito kwa viongozi wa vyama vya Ushirika kuhakikisha wanausimamia vizuri na kwa uaminifu mkubwa.

"Acheni kuwaibia wakulima na badala yake wasimamieni vizuri na vipimo viwe vya uhakika. Wanapoleta mazao yao maghalani msiwaibie,"alisema.

Alisema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ameweka nguvu kubwa katika sekta ya kilimo, lengo ni kuifanya Tanzania kuwa mzalishaji mkubwa wa mazao ya chakula na biashara, hivyo watendaji wahakikishe kinasimamiwa vizuri kuongeza tija.

Alisema Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia, inaendelea kuimarisha huduma mbalimbali za kijamii katika maeneo yote nchini.

Majaliwa alisema huduma hizo ni pamoja uboreshwaji wa miundombinu ya elimu, afya, maji, nishati na barabara.

SHERIA

# Ponda atangaza msimamo mpya, Polisi Dar yajibu

Fortune Francis, Mwananchi
ffrancis@mwananchi.co.tz




Katibu Mkuu wa Shura ya Maimamu, Sheikh Ponda Issa Ponda akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu nia yao ya kuandaa upya maandamano ya amani ya kupinga mauaji ya raia nchini Palestina. **Picha na Michael Matemanga**

**Dar es Salaam.** Siku mbili baada ya kuachiwa kwa dhamana Katibu Mkuu wa Shura ya Maimamu, Sheikh Ponda Issa Ponda, amesema bado wana dhamira ya kufanya maandamano ya kitaifa yatakayohusisha taasisi mbalimbali.

Novemba 10, 2023 Sheikh Ponda na baadhi ya wanachama wa taasisi hiyo walikamatwa na Jeshi la Polisi walipokuwa wakijiandaa kuandamana kutoka Mnazimmoja hadi Manzese kwa lengo la kuhamasisha kusitishwa kwa vita kati ya Israel na Palestina.

Awali Kamanda wa Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, Muliro Jumanne alitangaza kupiga marufuku maandamano hayo.

Jana alipotafutwa kuzungumzia suala hilo, Kamanda Muliro alimtaka mwandishi amtafute Msemaji wa Polisi, David Misime.

Akilifafanua, Misime alisema suala hilo halina masilahi ya Taifa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa, Sheikh Ponda alisema watahamasisha maandamano ili kufikisha ujumbe na ni haki yao kikatiba.

"Sisi hatuoni sababu ya kutoitumia njia hiyo, bado tuna dhamira ya kufanya maandamano yatakayokuwa ya kitaifa yatakayoshirikisha mashirika yanayotetea haki za watoto, wanawake, wazee na binadamu kwa ujumla," alisema Ponda.

Alisema wamekusudia kupeleka ushawishi kwenye taasisi mbalimbali ili kufanya maandamano makubwa ambayo yatakwenda kwenye Ubalozi wa Marekani au Umoja wa Mataifa kwa lengo la kufikisha ujumbe.

"Kuanzia leo tutaanza kufanya mawasiliano na taasisi hizo, ili kuangalia namna ya kuratibu suala hili, kwani kazi ya Jeshi la Polisi ni kusimamia sheria," alisema.

Alisema wanalaani na kupinga vikali kuzuiwa kwa maandamano yao, akidai kuwa walishatoa taarifa, "Tulitoa taarifa siku saba kabla lakini tulikaa kikao cha mashauriano, hoja zao walizozisema wamepata taarifa ya ugaidi, lakini sisi tukasimamia kwa kuwa wao jukumu lao ni kulinda raia na mali zao basi wazuie ugaidi huo," alisema.

Akizungumzia kuzuiwa kwa maandamano waliyopanga kufanya Novemba 10, Muliro alisema kwenye nchi hii huwezi kuruhusu kila kitu, unapokuwa na haki moja unatakiwa uangalie na haki nyingine.

> **"Kwenye nchi hii huwezi kuruhusu kila kitu, unapokuwa na haki moja unatakiwa uangalie na haki nyingine."**
> Murilo Jumanne

# Waziri Mkuu aonya migogoro ya wakulima, wafugaji nchini

Imani Makongoro, Mwananchi
imakongoro@mwananchi.co.tz



**Dar es Salaam.** Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa ameonya kuwepo kwa migogoro ya wakulima na wafugaji, akisema haina tija katika juhudi za kuleta maendeleo na kila upande unapaswa kujua kuwa hakuna mwenye haki zaidi ya mwingine.

Amesisitiza kuwa Serikali haitaki kuiona migogoro hiyo ikiendelea na kutaka kila upande uweke mpango kazi ambao hautaathiri mwingine.

Majaliwa alikemea hilo jana, alipokuwa akizungumza na wananchi wa vijiji vya Nanjaru wilayani Ruangwa Mkoa wa Lindi, akiwataka watendaji wa vijiji kabla hawajagawa maeneo kwa wafugaji wahakikishe idadi ya mifugo na washirikishe Serikali ya kijiji na wananchi.

"Kitendo cha wafugaji kuingiza mifugo kwenye mashamba ya wakulima ni uvunjaji wa sheria na Serikali haitavumilia vitendo hivyo.

"Wafugaji pia badilikeni fugeni kisasa, msione fahari kuwa na idadi kubwa ya mifugo ambayo mnashindwa kuihudumia, fugeni michache ambayo mtaihudumia vizuri na kuiuza kwa gharama kubwa," alisema Majaliwa.

Akiwa kwenye ziara ya kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa wilayani Ruangwa mkoani Lindi, Majaliwa alisema kilimo na ufugaji kwa pamoja ni maisha, biashara na fedha.

"Kila mkulima alime kulingana na ukubwa wa eneo lake na mfugaji afuge mifugo kulingana na ukubwa wa eneo lake na malisho, sote ni Watanzania na tunataka utajiri. Wakulima na wafugaji waheshimiane kwani wote ni Watanzania," alisema.

Wakati huohuo, Waziri Mkuu alitoa wito kwa viongozi wa vyama vya ushirika kuhakikisha wanasimamia vizuri na waache kuwaibia wakulima, badala yake wasimamieni vizuri na vipimo viwe vya uhakika.

"Wanapoleta mazao yao maghalani msiwaibie, Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan ameweka nguvu katika sekta ya kilimo, lengo ni kuifanya Tanzania kuwa mzalishaji mkubwa wa mazao ya chakula na biashara, hivyo hakikisheni mnasimamia vizuri ili kuongeza tija," alisema.

Zan…
na …

Aurea Sim…
asimtowe…

NYUMBA Y…
INATA…

Nyumba aina ya Villa ina…
katika eneo la Masaki kw…

- Iwe na eneo la ardh…
baina ya 1500 mpaka…
- Iwe mpya au imefany…
- Iwe na vitu vingine k…
mlinzi na choo cha n…
- Mmiliki wa nyumba…
sahihi mkataba wa…

IKIWA VILLA HIYO I…
YALIYOTAJWA MMIL…
ZIFUATA…
022 2150…

CamScanner